Ngurumo 27/4/63

## MKUTANO

Tunakuomba kuwa ututangazie kwa wanachama wote wa FRELIMO kuwa siku ya Jumaa Pili yaani tarehe 28/4/63 hapo penye ukumbi wa A. Community Centre patakuwa na mkutano wa hadhara, tangu saa nane za mchana mpaka saa kumi na mbili jioni.

Kati ya watu watakaohutubia pia atakuwapo Makamu wa Rais wa chama, Mheshimiwa Padre Simango, basi jamaa wasikose mambo maalumu siku hiyo.

Natia mkazo kusema kwamba tujiunge kwa njia ya Frelimo tukiwa tuna sauti ya Frelimo, kusema kweli, chama cha Frelimo ni chama kinachoongozwa na Dr. Mondlane, na ndicho kijulikanacho ulimwengu mzima.

Wananchi wote wa Mozambique hatuna budi kuungana na Frelimo, na kama hujawa bado mwanachama ingia sasa hivi. Hatuna budi kufuata uongozi wa Dr. Mondlane. Mtu ye yote atakayekiacha chama cha Frelimo, aatambue wazi kuwa ana matumaini ya kuunda chama cha kupoteza wakati wa Wananchi, na watakaofuata mtu kama huyo itaonyesha waazi kuwa amepokea mlungura kutoka Ureno.

Mitaani kunasemeka na kuwa kuna baadh ya watu fulani wanac kataa uongozi wa D Mondlane ili kutaka k chelewesha uhuru na k zidi kumpa nguvu Mre no kuwauwa na kuwa tesa Wananchi. Nasem wazi kuwa vibaraka h o ni watu wanaopend kushiba wenyewe, n kupendelea Wananc wengi kuuawa na kuz di kuteswa. Epukana n vibaraka hao na unga na na Frelimo upes ili tuulete uhuru. Vib raka hao tunawafaha mu na maamzi yao ya ko karibuni. Tunach mba kaburi la kuwa ka sasa.

Khamisa Fundi,
Keko Mwanga,
Dar es Salaam.